


# Uhuru na Amani

GAZETI LA KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA TOLEO LA 4, 2013 Bei Sh. 500



Vol. 113, Toleo la 4, 2013

50

ISSN 0856 - 1214

# Upendo FM 107.7



*Amani kwa wote*

JE UNAFAHAMU KITUO BORA CHA REDIO KATIKATI YA JIJI?

Kwa matangazo ya biashara na mikutano ya Injili,  
kwa ushauri wa kiroho na maendeleo ya jamii:  
Tangaza kwenye Redio bora ya Upendo na Amani  
kwa wote.

Fika sasa **LUTHER HOUSE**  
**GHOROFYA PILI**  
**SOKOINE DRIVE.**

Upendo FM 107.7 MHz  
P.O. Box 13603  
Da es Salaam, Tanzania

Simu: 022 212 4228/ 2139556/ 2124221  
E-mail: upendofm@yahoo.com



## Ifahamu

### RADIO SAUTI YA INJILI

FM 92.2 & 96.2 MHz  
MOSHI

RSYI ni rafiki anayekujali kiroho na kimwili.

Katika Masafa ya FM, Radio Sauti ya  
Injili kutoka Moshi inasikika vizuri  
kabisa katika Masafa yafuatayo:

Moshi	92.2 MHz	Mlalo (Lushoto)	102.6 MHz
Arusha	96.2 MHz	Kisosora (Tanga)	96.7 MHz
Same	100.4 MHz	Morogoro	96.6 MHz
Kibaya (Kiteto)	102.9 MHz	Hakwe (Rombo)	96.4 MHz

Aidha Radio Sauti ya Injili, Moshi inasikika kwenye  
tovuti dunia nzima kwa saa 24  
[www.sautiyainjili.org](http://www.sautiyainjili.org)

Radio Sauti ya Injili inatangaza vipindi  
mbalimbali vikiwemo vya maendeleo,  
afya, uchumi, habari na halikadhalika  
vipindi vya mafundisho ya dini. Unaweza  
kupata habari moto moto za kitaifa na  
kimataifa katika kipindi cha Dira ya Leo.

Wasiliana na:  
Mkurugenzi RSYI  
S.L.P. 777, Moshi

Simu: 027 27 52772 au 027 27 53080  
E-mail: [redio@elct.org](mailto:redio@elct.org)  
Tovuti: [www.sautiyainjili.org](http://www.sautiyainjili.org)

Kumbuka kuwa RSYI ipo kwa ajili yako. Aidha,  
kijamii. Endelea kuimarisha huduma nzuri hii kwa  
hali na mali.

## Radio Furaha 96.7 FM

**Sikiliza matangazo ya  
kituo bora cha Redio Iringa  
na maeneo jirani.**

Kwa maoni, ushauri wa kiroho  
na kijamii wasiliana na:

**Meneja: Protas Kanemela**  
**Simu: +26 27 003 43**

**Fax: +255 262 701 198**

**Barua pepe: [elctrdrd1987@yahoo.com](mailto:elctrdrd1987@yahoo.com)**



Uhuru na Amani ni Gazeti la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Hutayarishwa na Kitengo cha Mawasiliano, KKKT.

Maoni yaliyomo katika makala zinazochapishwa ni ya mwandishi anayehusika na wala hayawakilishi mawazo ya Kanisa ama mhariri isipokuwa pale ambapo imetamkwa wazi.

Ukiwa na maoni, ushauri, makala au maswali mwandikie:

**Mhariri**  
**Uhuru na Amani**  
**S.L.P. 3033**  
**ARUSHA**

**Barua pepe:** elobulu@elct.or.tz  
**sms kwa Mhariri:** 0754-482-285

**Fungua Tovuti ya KKKT:**  
<http://www.elct.org/>

## **MHARIRI** **Elizabeth Lobulu**

Newspaper Design & Typesetting:  
**Elizabeth Lobulu**

Limepigwa Chapa na:  
**Moshi Lutheran Printing Press**  
S.I.P 301 Moshi  
lutheranpress@yahoo.com

### **Wachangiaji wa Makala:**

Prof. Wilfred Mlay  
Askofu Dkt. B. K. Bagonza  
Askofu Dkt. S. Mushemba  
Mch. Dkt. Wilson Niwagila  
Mch. Dkt. Elieshi Mungure  
Samwel Kasigwa Kayanda  
Philemon Mark Fihavango

Deo Mosh

Hellen Madege Yongo

Jacklin Materu

Zawadi Mchome

Mch. Dkt. Faith Lugazia

Mch. Prof. Festo Bahendwa

### **Wapiga Picha:**

Michael Shayo (KKKT)  
Heidi Martinussen (FMKD)  
Antje Lanzendorf  
(Misioni ya Leipzig)

# **MAONI YA MHARIRI**

Tanzania inasifika kwamba ni nchi yenyewe amani barani Afrika. Amani hiyo inatokana na juhudini kubwa za wananchi wenye na viongozi wao ambao wamekuwa siku zote wakipigania umoja na mshikamano licha ya tofauti zao.

Matatizo yatakuwepo siku zote lakini yasitufanye tuache misingi ya amani, utulivu na mshikamano wa kindugu tuliokuwa nao baada ya uhuru. Moja ya tatizo linalokumba taifa letu kwa sasa ni mmomonyoko wa maadili. Na hili lilifanya Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira kianzishe mafunzo maalumu ya maadili kama sehemu ya mitaala. Tunatoa pongezi kwamba jambo hili limefanyika wakati muafaka. Lengo la kozi ni kumwandaa mwanafunzi awe mkamilifu kimwili, kiakili, kiroho na kisaikolojia katika kukabiliana na hali za maisha yake ya kila siku.

Wahadhiri wa Chuo hicho walipopata nafasi wakati wa Kongamano la Jubilii ya miaka 50 ya umoja wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) walisema: viashiria au dalili za mmomonyoko wa maadili ni pamoja na taarifa za mauaji ya vikongwe kwa sababu za kishirikina; mauaji ya viongozi wa dini; mateso na ukatili kwa wanawake, watoto, maalbino, waandishi wa habari, kutekwa na kujueruhija kwa viongozi wa vyama vya hiari, nk.; migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji; matukio ya kulipua au kuchoma moto makanisa, kuenezwa kwa kasi maambukizi ya Virusi vya Ukimwi; matumizi ya madawa ya kulevyia; matumizi mabaya ya teknolojia ya habari; ongezeko la umaskini katika jamii; na maovu mengine mengi. Hivi karibuni tumeshtushwa zaidi kwamba wako watu wanaofundishwa ugaidi kupidia kundi la Al Shabab. Huko Mtwara walikamatwa vijana wakiwa katika kambi msituni wakijifunza ugaidi na huko Kilindi mkoani Tanga kuna watoto na vijana waliokutwa kambini. Haya yote yangeweza kuepukwa endapo maadili yasingekuwa yamemomonyoka.

Kwa kuwa chuo cha Kanisa hutoa mafunzo ya kozi mbalimbali bila ubaguzi tunaamini kwamba kozi ya maadili itaweza kusaidia angalau kutoa makundi ya wahitimu wenye maadili mema kwa maendeleo ya jamii na taifa letu ili kudumisha amani iliyokuwepo tangu uhuru.

Kila mtu anatakiwa kutimiza wajibu wake katika kuwakuza watoto wawe na maadili mema kwani si kila mtu atapata fursa ya kwenda kusoma katika Chuo cha KKKT. Tujifunze toka kwa nchi jirani kwamba ubaguzi wa kikabila unaweza kufikisha jamii katika mapigano, hata ya kimbari. Hivyo tuhimize umuhimu wa umoja, utengamano na utulivu ili Tanzania iendelee kuwa nchi ya amani.

### **PICHA YA JALADA:**

Kilele cha Jubilii ya miaka 50 ya umoja wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) kiliadhimishwa kwa Ibada iliyofanyika Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira 23 Juni 2013. Pamoja na mambo mengine, Mkuu wa KKKT Askofu Dkt. Alex Gehaz Malasusa, alizindua Kitabu: "Umoja na Utambulisho Wetu". [(c) 2013/ KKKT/ Picha na Michael Shayo].

# Askofu ataja vipaumbele vya Kanisa

Wakati wa jubili ya miaka 50 ya umoja wa KKKT, liliandaliwa Kongamano Chuoni Makumira 22 Juni 2013. Ufuatao ni ufupisho wa mada kuhusu 'Misioni ya Kanisa Miaka 50 Ijayo'.

NA ASKOFU DKT. BENSON BAGONZA

## Habari Njema itangazwe kwa upya

Baada ya kipindi cha kueneza Ukristo inaelekea ushuhuda mionganini mwa *wakristo kuwa chumvi na mwanga* ulipotea. Ukristo jina ulipenya polepole na kupoteza mapokeo yaliyoensi ya maana ya kuiishi *Ukristo wa kweli*. Katika familia za Kikristo kuna kila aina ya uovo kama vile vitendo vya rushwa; ushoga na ulawiti; kutazama kanda au picha chafu za kujamiihana; ubaguzi wa rangi; maisha ya upotofu, mauaji ya kimbari, nk.; bila kuona kwamba mambo hayo ni mwiko katika familia za kikristo. Watu hao wamebatizwa na kupoakea Kipaimara na bado wako katika orodha ya Washarika hai lakini hao, nionavyo mimi; wawekwe katika *eneo la misioni ndani ya makanisa yetu*.

## Misioni shirikishi:

Tu watendakazi shambani mwa Mungu. Hakuna mtazamaji na hakuna kabilia lililo juu ya jingine katika kuisimamia misioni ya Mungu. Je haya ndivyo yanayoonekana kutendeka? Ni lazima mahusiano kwa wanaopelekewa Injili na wanaopokea Injili yabadilike na kujengwa katika hali ya usawa na uangavu katika mambo yahusuyo misioni. Inabidi kutafuta njia za kuziba nyufa zinazotubagua kwa tofauti za jinsi, rika, teknolojia, kiuchumi, eneo la kijirografia, nk.

## Misioni iwe ya Kinabii:

Utandawazi umehamisha wajibu wa kinabii toka mkononi mwa makanisa na kuweka uwezo huo mikononi mwa mashirika yasiyo ya kiserikali na vyama vya hiari vya kijamii. Mafundisho ya Kanisa hayana mguso wa 'ukali' kama ilivyokuwa zamani na pale ambapo yanaonesha ukali kila aina ya njama hutumika kunyaamazisha Kanisa. Kama kanisa ni tegemezi kiuchumi

halitafaulu sana kutoa sauti ya kinabii. Uwezo wa kifedha kama vile *Euro* na *Dola* utachukua nafasi ya uwezo wa *Neno la Mungu* uliokuwa unalifanya kanisa liwe na sauti ya unabii. Hili ni eneo muhimu kwa KKKT kwa kuwa tuna majukumu mawili. Tunawiwa kushuhudia wenzetu wa nchi zillizoendelea pamoja na jamii yetu ilijoaa rushwa na pia tunapaswa kuichunguza hata miundo ya kikanisa.

## Misioni ni maridhiano:

Utandawazi unaonesha kwamba hakuna aliye na uwkeli wote kuhusu mambo ya imani. Lakini Kanisa limeweka imani yake *katika haki ya Kristo aliye njia, kweli na uzima*. Hata hivyo, katika maeneo muhimu masuala ya Ukristo hayachukui nafasi kwamba ni dini kuu. Na hii ni changamoto kwa mikakati ya maeneo mapya ya misioni. Lazima tujifunze kukubali kuwepo kwa hali tusiyozea kuibadilisha tunavyopenda. Hivyo inabidi tukubali kujadili, kuridhiana na kukubaliana kuendea masuala ya misioni katika maeneo mapya kwa muktadha wa maridhiano.

## Ibada za nyumba kwa nyumba:

Muundo wa KKKT unaonesha kwamba 'nyumba' ni kanisa katika ngazi ya mwanzo. Hata hivyo, muundo unaoonekana wazi zaidi katika ngazi ya usharika ambapo watu hukutana tu kwa ajili ya Ibada ya Jumapili japo wote ni kutoka kijiji au mtaa mmoja. Hivyo, masuala ya imani si sehemu ya ajenda za kila siku katika eneo la kazi, mikutano ya vitongoji, nk. **Inabidi kuiishi Neno na Sakramenti** tangu ngazi ya nyumba na kijijini kwa njia ya 'ibada za nyumba kwa nyumba.' Tumeanza haya KKKT Dayosisi ya Karagwe miaka mingi



Askofu Dkt. Benson Bagonza,  
KKKT Dayosisi ya Karagwe.

iliyopita na matokeo ni dhahiri.

## Misioni kupitia watoto:

Utandawazi umebomoa kuta za familia. Si rahisi tena kukuta familia nzima iko mezani kwa chakula cha mchana au cha usiku kila siku. Watoto hawako tena nyumbani kwa ajili ya masomo kuanzia ngazi ya chekechea hadi vyuo vikuu. Wasaidizi wa nyumbani (mayaya) ndio wanaka na watoto muda mrefu kuliko wazazi wao. Mabadiliko haya ya haraka ya mfumo wa kifamilia hayataacha kuathiri Kanisa na jamii kwa jumla; na hili ni eneo jipya la kufanyiwa misioni.

## Mabadiliko ya hali ya hewa:

Hali ya hewa imebadilia. Badiliko hili limepewaa majina mengi na dhana nyingi. Bila shaka mabadiliko hayo yanabadili kila kitu bila ubaguzi. Inatualika kushiriki kukabili hali hiyo kama eneo letu jipya la misioni. Kutokana na tatizo hili uumbaji wa Mungu umeathirika kwa kutishia haki za binadamu kutoka kwa Mungu; yaani maji, ardhii, masuala ya ekolojia na haki ya kufaidika na hewa inayozunguka dunia. Hili ni eneo jipya la misioni ya KKKT lakini itabidi kuliingia kwa ujasiri na kujamini. Kwa kuwa ni jambo ligusalo nyanja nyininge limeathiri pia masuala ya afya, tiba, elimu na diakonia.

## Ni Nsanganelu Mbulu

Mch. Nicolaus Nsanganelu anatarajiwaa kuwekwa wakfu kuwa Askofu wa KKKT Dayosisi ya Mbulu, mnano 19 Januari 2014 kuchukua nafasi iliyoachwa na Askofu Zebedayo Daudi ambaye amestaafu. Mch. John Nade anakuwa Msaidizi wa Askofu kuchukua nafasi ya Mch. Nsanganelu.

## Mkatabana Kanisala Bavaria

Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa, alitia saini Mkataba wa Mahusiano baina ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Bavaria na KKKT 23/6/2013. Mkuu wa KKKT Askofu Alex Malasusa na viongozi wa Kanisa la Bavaria walishuhudia. Dkt. Dorothea Deneke-Stoll ambaye ni Mwenye Kitawo Sinodi Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Bavaria alisaini kwa niaba ya kanisa lake.



## Chuo Kikuu cha Iringa chazinduliwa, chatunukiwa tuzo

Chuo Kikuu Kishiriki cha Iringa kuanzia mwaka wa masomo 2013/14 kinajitegemea na kujulikana kwa jina: "Chuo Kikuu cha Iringa". Uzinduzi wa Chuo hicho ulifanyika wakati wa sherehe za Mahafali ya 16 ya Chuo Oktoba 2013. Chuo hicho kilianza 1994 kama moja ya matawi ya Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.

Chuo hiki ni cha pili kati ya vyuo vishiriki nya Tumaini ambavyo vimekuwa vyuo vinavyo jitegemea. Chuo Kikuu Kishiriki cha Sebastian Kolowa kilichoanza 2007 kilikuwa cha kwanza kujitegemea tangu 2012. Kwa maelezo zaidi fungua [www.makumira.ac.tz](http://www.makumira.ac.tz)



Prof. Nicholaus Bangu, Makamu Mkuu wa Chuo cha Iringa akiwa na "Tuzo ya Heshima ya Sheria za Vita" ambayo chuo hicho kimeshinda nafasi ya kwanza katika mashindano yaliyoshirikisha nchi saba za Afrika. Chuo kilikabidhiwa tuzo hiyo jijini Arusha Novemba 2013.



Bibi Faustina Nillan,  
Mkurugenzi Kazi za  
Wanawake na Watoto KKKT.

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania tarehe 16 Novemba 2013 lilikabidhi rasmi Mradi wa maji ulioharimu sh. milioni 37 kwa wakazi wa Kijiji cha Chilungulu Dodoma.

Mkurugenzi wa Kazi za Wanawake na Watoto KKKT, Bibi Faustina Nillan, alimweleza mgeni rasmi kwamba KKKT kwa kushirikiana na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Marekani limetoa fedha hizo ili kununua pampu, nyaya, genereta na malipo ya kazi. Kazi ilisimamiwa na Mhandisi wa Maji Wilaya ya Bahi, Injinja Deus McHele. Kijiji hicho kipo Wilaya ya Bahi, Dodoma. Mradi huo wa maji ni ombi la wanakijiji cha Chilungulu ambaa wametoa

Bibi Faustina Nillan aliajiriwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) Julai Mosi 2013 kuwa Mkurugenzi mpya wa Kazi za Wanawake na Watoto KKKT kuchukua nafasi iliyoachwa na Bibi Rachel Ramadhani ambaye alitumikia Kanisa katika nafasi hiyo tangu 1994 hadi 2013.

Bibi Nillan ana uzoefu wa

## Mradi wa maji Chilungulu wakamilika

ekari 300 za ardhi ili Kurugenzi ya Wanawake ijenge Kituo cha Mafunzo na Mikutano.

Akiuzindua mradi huo wa maji, Askofu Amon Kinyunu, Mkuu wa KKKT Dayosisi ya Dodoma, aliwaasa wanakijiji wasimamie vizuri mradi huo na kulinda vifaa ili mradi huo uwendelevu. Pia alisema ingefaa uongozi uorodheshe wazee waliopo waweze kupata maji bure.

Makabidhiano hayo yalihudhuriwa na Bw. M. W. Mallumbo, Naibu Katibu Mkuu Mipango na Maendeleo KKKT; Mch. Rachel Axwesso, Naibu Katibu Mkuu Huduma za Jamii na Kazi za Wanawake KKKT; Bibi Rachel Ramadhani

## LMC yapata Katibu mpya

Bw. Peter Karlsson tokwa Sweden ameteuliwa kuwa Katibu wa Lutheran Mission Cooperation (LMC) kuanzia Januari Mosi 2014 kuchukua nafasi toka kwa Mratibu wa Muda Bibi Byera Herman. Mwaka 1987 - Desemba 1992 Bw. Karlsson alitumikia KKKT Dayosisi ya Kusini na 2002 - 2006 alifanyakazi KKKT Dayosisi Mashariki ya Ziwa Victoria.

Akiwa Dayosisi ya Kusini Januari 1987 - Juni 1988 alikuwa Mhasibu; Julai 1988 - Aug. 1990 Mtunza Hazina na Sept. 1990 - Desemba 1992 Mkaguzi wa Ndani.



Bw. Peter Karlsson  
Katibu wa Lutheran Mission  
Cooperation (LMC).

Katika Dayosisi Mashariki ya Ziwa Victoria 2002 - 2004 alikuwa Mshauri wa Fedha na Mkaguzi wa Ndani na Mei 2006 - Novemba 2006 alikuwa Mshauri wa Fedha.

Sekondari Weruweru na Shule ya Sekondari Mawenzi zote za mjini mkoani Kilimanjaro.

Hafla ya kumuaga Bibi Ramadhani ilifanyika 30 Oktoba 2013 ambapo watumishi wengine watatu waliostaafu nao waliagwa: Hao si wengine ni Mzee Emmanuel Madebe, Naftal Siaiti na Meseyeki Long'amu wa Idara ya Utawala.

aliyekuwa Mkurugenzi wa Kazi za Wanawake KKKT na Wajumbe wa Halmashauri

ya Wanawake toka Dayosisi za KKKT ambaa walikuwa Dodoma wakihudhuria warsha.



Kikundi cha ngoma kikiwatumbuiza watu waliofika katika makabidhiano na uzinduzi wa Mradi wa Maji Chilungulu.

# Ni muhimu kufundisha maadili - Prof. Bahendwa

**Na Mchg. Prof. Lutashumululwa  
Festo Bahendwa,  
JOKUCo.**

Kama ilivyo kwa jamii ya Tanzania, wanafunzi wanaojinga na Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira (TUMA) wana malezi tofauti tofauti kutokana na makabila yao, imani zao za kidini na za kisasa, na mahali walikokulia (mjini au kijiji). Hali hii pamoja na uwepo wa ugonjwa hatari wa UKIMWI ni mojawapo ya mambo yanayoshuhudia kwamba katika nchi yetu suala la maadili ni 'jangalita'.

Mambo mengine yanayoonesha kuperomoka kwa maadili ni kuwepo kwa rushwa iliyokithiri; mauaji ya vikongwe kwa tuhuma za kishirikina; mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi (maalbino); migogoro ya kidini; migogoro ya ardhi; mapigano kati ya wafugaji na wakulima; utumiaji wa madawa ya kulevyo; matumizi mabaya ya teknologia ya kisasa; umaskini uliokithiri mionganoni mwa Watanzania wengi; vitendo vingi vya uhalifu, n.k.

Somo la "Misingi ya Imani na Maadili" limeingizwa katika mitaala ya Chuo ili kuwaandaa wanafunzi kuwa viongozi wenye maadili mema katika jamii. Kupitia somo hili vijana wanaandalia kuwa raia wema, watu wenye uzalendo, wenye moyo na ari ya kupenda kujenga nchi kwa manufaa ya raia wote. Lengo la somo si kuwaongoa au kuwafanya wanafunzi wasio Wakristo kuwa Wakristo.

Shabaha ya somo ni: Kuwaandaa wanafunzi katika ukamilifu wa utu wao: kimwili, kiroho, kiakili, na kisaikolojia ili wakabiliane vema na masuala magumu yahusuyo imani zao, maadili ya kazi zao, na maisha yao binafsi.

Shabaha nyingine ni kuwaongoza na kuwawezesha wanafunzi kufanya maamuzi sahihi ya kimaadili katika maisha yao. Hapa maamuzi sahihi ni yale yasiyoleta madhara, maumivu, au majuto kwa mwanafunzi mwenyewe na kwa watu wengine.

Pia somo linalenga kuwajengea wanafunzi uwezo na waweze kuwa watu wenye maadili mema yatokanayo na msukumo wa ndani ya dhamiri zao badala ya kutenda mambo kinafiki kwa kuongozwa na msukumo wa nje unaojali kuwardihisha watu fulani tu.

Kupitia somo hili, wanafunzi wanaongozwa na kuhimizwa kujitahidi wakati wote kutenda mema na kujizua kutenda maovu. Wanafunzi wanahimizwa kuzingatia fundisho kuu kuhusu maadili: "Basi yo yote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo" (Mathayo 7:12).

Aidha kwa njia ya somo la maadili, wanafunzi wanahimizwa kuonesha upendo kwa watu wote hata kwa adui zao. Jambo hili ni muhimu hasa katika

mazingira ya sasa ambapo vitendo viovu vinafanya kwa uwazi, dhidi ya wengine. Katika mazingira ambapo kwa kisingizio cha kutetea imani watu fulani wanachoma majengo ya ibada, wanaharibu mali ya wengine, na wakati mwingine kwa sababu zisizo jukumu kuteka, kutesa, na kuua wengine, wazo la kumpenda adui linapaswa kupewa umuhimu wa pekee.

Japo nimejadili kuhusu vijana au rika la ujana lakini haina maana wao wamesababisha mmomonyoko wa maadili bali wao ni nguvu ya mabadiliko ya haraka inayoletwa na: Wimbi la makundi makubwa ya watu kuhamia mijini; maendeleo ya kiuchumi au kurudi nyuma kimaendeleo na upatikanaji taarifa zisizo na kifani hasa katika mitandao ya mawasiliano. Utandawazi umeathiri fikra, matendo na mitindo ya maisha ya kila mmoja katika jamii zetu.

Faida nyingine ya kozi ya maadili ni kwamba wahitimu wanajenga tabia ya kujiheshimu, kuheshimu wengine, kuwajibika kama raia na kuheshimu mazingira ya asili. Wakufunzi wa vyuo vikuu inapasa waweze kuingiza tunu za mambo haya kwa ujumla wake katika masomo yote katika mitaala ili kuwasaidia wanafunzi wajue wajibu wa kutumikia jamii kwa vitendo.

Na yote wakufunzi wanayowafundisha darasani ni lazima yaonekane dhahiri katika maisha na matendo ya walimu wao nje ya darasa ili kuwa kielelezo au mfano wa kuigwa na wanafunzi wao.

Hatimaye wanafunzi watatfsiri kwa vitendo mawazo waliyojengewa ya kuwa na tabia na maadili mazuri yanayokubalika katika maisha yao ya kila siku na katika maeneo yao ya kazi.

Mwisho, ningependa kutoa changamoto kwa wasomi nichini Tanzania hasa vyuo vya juu na vyuo vikuu kwamba navyo vitekeleze jukumu la kuwaelimisha vijana masuala ya maadili. Kwa mfano: mawakili, walimu, wataalamu walibobe, mameneja na viongozi wawe ni watu wenye kujiheshimu na kuingoza Tanzania irudishe sifa ya kuwa nchi yenye kuthaminiwa, yenye usawa na uhuru. Inabidi watu waondokane na udikteta, maonevu, woga na mateso.



Askofu Dkt. Israel-Peter Mwakyolile (Kulia) na Mch. Prof. Joseph Parsalaw Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira wakiratibu Kongamano la Miaka 50 ya umoja wa KKKT. Mada tano zilitolewa.

## Askofu Kinyunu akabidhi mradi



Hivi karibuni Askofu Amon Kinyunu (KUSHOTO), Mkuu wa KKKT Dayosisi ya Dodoma, alizindua na kukabidhi Mradi wa Maji katika Kijiji cha Chilungulu Wilaya ya Bahi, Mkoani Dodoma. Kulia ni Mwenyekiti wa Kijiji hicho Bw. Charles Andrea. (PICA NA FAUSTINA NILLAN).

## Nelson Mandela hatunaye

Hadi tunaenda mitamboni dunia ilikuwa inamilia Nelson Mandela au 'Tata Madiba' ambaye alitwaliwa 5 Desemba 2013 akiwa na umri wa miaka 95 na kuzikwa 15 Desemba 2013. Mandela, mpigania uhuru na Rais wa kwanza mweusi wa Afrika Kusini huru 1994 - 98; Alikuwa mtu mashuhuri duniani kwa kupigania haki na kipinga siasa za ubaguzi wa rangi (apartheid) nchini mwake na duniani kwa jumla.

# Jukwaa la Ardhi laundwa

Na Elizabeth Lobulu

Kwa mafanikio makubwa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Sebastian Kolowa (SEKOMU) liliandaa mukutano wa kimataifa wa siku tatu kuhusu: "**Haki ya ardhi kwa amani endelevu Tanzania**," uliofanyika jijini Dar es Salaam tarehe

10 – 12 Septemba 2013. Kauli mbiu ilikuwa: "*Ardhi Yetu, maisha Yetu, Uhai Wetu.*"

Mkutano huo uliunda **Jukwaa la Ardhi** linalokusudia pamoja na mambo mengine kushiriki katika masuala ya uhifadhi wa mazingira na kutafuta njia za amani za kusuluhiha migogoro ya ardhi ikiwemo inayotokana na uwekezaji.



Askofu Dkt. Steven Munga  
Mwenyekiti wa Mkutano aliyeongea  
kwa niaba ya Mkuu wa KKKT.



Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa, (Wapili kushoto) akishiriki katika mukutano wa ardhi.

## Kanisa lataka amani endelevu

Mwenyekiti wa Mkutano huo, Askofu Dkt. Stephen Munga ambaye pia alimwakilisha Mkuu wa KKKT, alisema lengo la mukutano lilikuwa ni kuhamasissha majadiliano ili kuona jinsi ya kukabili migogoro ya ardhi baina ya wananchi na wawekezaji kwa njia ya amani.

Mkutano ultoa fursa ya kipekee kwa kufaulu kuwakutanisha wajumbe na wadau wengine wakiwemo viongozi watendaji wa Serikali, mashirika ya kiimani, wasomi, watafiti, wana vyuo, wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, wanasiasa, wawakilishi wa mabalozi, wafanyakishara, wawakilishi wa vyama vya kijamii, wakulima, wafugaji, wana harakati na wana habari.

Wajumbe hao wapatao 200 walipata matokeo ya tafiti na kubadilishana usoefu kuhusu masuala ya kumiliki rasilimali ardhi, Sera na Sheria za Ardhi



Waziri Mkuu Mhe. Mizengo Peter Pinda

nchini na za nchi nyingine Afrika.

Mada toka nchi kadhaa za Kiafrika zilionesha jinsi nchi hizo zinavyokabili masuala ya ardhi: umiliki, fidia kwa ardhi iliyotolewa kwa uwekezaji,

migogoro, nk.

Kwa kuwa nchi yetu inategemea kilimo kuwa ndio uti wa mgongo wa kiuchumi; ardhi ni kitu muhimu sana kwa mamilioni ya Watanzania. Washiriki wa mukutano walisema haki ya ardhi ni haki ya binadamu, hivyo walitaka hilo litamkwe katika Katiba Mpya inayoandaliwa.

Karibu kila kiongozi wa Serikali aliyeypata nafasi ya kuhutubia wajumbe alisema hakuna uporaji wa ardhi Tanzania kwa vile Sera na Sheria za ardhi zinazuia hilo lisiweze kufanyika.

Akifungua mukutano huo Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, aliahidi kutoa ushirikiano na kueleza utayari wa Serikali kulinda haki ya umiliki na kutumia ardhi kwa watu wake ili ardhi wanayomiliki iwe baraka na na wala 'isiwe laana' kwao.

# Kuna wimbi la kusaka ardhi

Kuna wimbi liendalo kasi la umiliki wa ardhi kibiashara nchini Tanzania kama ilivyo katika nchi nyingine za Kiafrika. Makampuni na wafanyabiashara matajiri wa ndani na nje ya nchi wananchi na maeneo makubwa ya ardhi kwa lengo la uwekezaji au ‘kulangua’ endapo bei itapanda kwa siku zizazo. Matatizo katika matumizi ya ardhi si kutokana na wawekezaji wa nje tu bali hata mgawanyo wa matumizi ya ardhi ni tazizo.

Prof. Aidan G. Msafiri akiwasilisha mada kuhusu “*Tafsiri mpya kuhusu maadili na haki katika matumizi ya ardhi Tanzania*,” alisema mbio za kushindana kutwaa ardhi, zina msukumo wa dhana ya kutengeneza faida katika mfumo wa utandawazi duniani; ambapo ni dhahiri kwamba uwezo wa kiuchumi unategemea hati za umiliki wa ardhi na rasilimali nyingine kama vyanzo vya maji, nk. Alisema “baadhi ya walio maskini sana Tanzania wanapoteza haki ya kumiliki ardhi yao ya jadi; vyanzo vya maji na rasilimali nyingine ambazo hapo awali walizituma kuendesha maisha yao tangu kizazi cha enzi za mababu zao.

Prof. Msafiri alisema japo uwekezaji huo unahesabiwa kwamba ni mbinu ya ‘kuondoa umaskini;’ hilo si lengo rahisi kufikia. Kama kweli lengo ni kutoa ajira ni watu wachache tu wanawenza kuajiriwa kwa malipo ya chini sana. Pia kutokana na misamaha ya kodi kwa wawekezaji, ‘mapato kwa Serikali ni hakuna,’ alisema.

Akitoa mada kuhusu “*Biasara ya zao*

*la Jatrofa (mibono) Nchini Ghana*,” Dkt. Festus Boamah, alisema ongezeko la ghafla la ugawaji ardhi kwa wawekezaji barani Afrika na maeneo mengine linasababishwa na msukumo wa vitu vitatu: *chakula, nishati na rasilimali*. Je, kati ya mambo hayo, nani hasa anafaidika? Kiuhalisia, chakula na nishati ni kwa ajili ya kuza nje na si kwa ajili ya wananchi; na rasilimali pamoja na fedha toka mabenki, zinazotolewa kwa wawekezaji wa nje, au rasilimali huporwa na kusafirishwa na wawekezaji kwenda nje ya nchi.

Alisema istilahi kama ‘uporaji wa ardhi’, ‘umiliki ardhi’ au ‘biasara ya ardhi’ zote zina maana inayolingana. Tofauti ni kwamba inategemea nani anatumia istilahi hizo. Kwa mfano, mwekezaji

atasema ni ‘*namiliki ardhi kibiashara*’. Mtumishi wa Serikali atasema ni utoaji na upatikanaji wa ‘*miliki ya ardhi*’. Kwa upande wa aliyedhulumiwa ardhi ataona hu ni ‘*uporaji wa ardhi*’.

Wanaharakati na watafiti wanasema hali halisi inaonesha kwamba si kila uwekezaji ni jambo jema na lenye manufaa. Na vilio vya wananchi vinavyosikika kila eneo nchini vinaashiria wasiwi katika utekelezaji wa taratibu za utoaji wa ardhi kubwa sana kwa wawekezaji; kwamba liwe ni jambo la kufuatiliwa kwa makini. Kwa upande wake Kanisa linatetea wananchi wapewe haki kumiliki na kutumia ardhi na fidia stahili pale ardhi yao itamilikishwa watu wa kutoka eneo jingine au wageni toka nje kwa lengo la uwekezaji.



## Matatizo yako maeneo mengi - wajumbe

Akiwasilisha mada kuhusu “*Vikumbo kugombea ardhi barani Afrika*,” Prof. Sam Moyo toka Zimbabwe alisema uporaji ardhi kama upo, au ni madai tu; ni jambo ambalo si la hapa Tanzania tu, bali jambo hilo lipo katika nchi nyingine zilizoendelea. Katika Karne ya 19 wakoloni wa ulaya walipigana vikumbo kugombea mashamba na maliasili ya Afrika na kuligawa bara hili vipande vipande ili kurahisisha uporaji wa mali asili zetu. Ni kwa kugawanya huko ndipo Tanganyika na baadaye Tanzania ilipozaliwa.

Washiriki wa mukutano walisema pamoja na kwamba nchini kuna haki ya kupata fidia kwa mujibu wa Sheria Namba 4 ya Ardhi ya Mwaka 1999; lakini haki haitendeki kwa watu wanaopoteza ardhi yao kwa kukosekana uangavu katika mchakato wa mashauriano (mikataba) na kubainisha nini kiwango halisi cha fidia hivyo kusababisha migogoro ya ardhi.

Haieleweki kwa nini mwekezaji anatakiwa alipe sehemu kubwa ya fidia kwa vyombo vya dola kama manipaa au halmashauri badala ya fidia hiyo

kulipwa wahuksika waliota ardhi vijiji. Fidia huchukua muda mrefu tangu makadirio ya fidia yafanyike hadi pesa inapotolewa hivyo thamani halisi ya fedha zilizokadiriwa inakuwa imeshuka.

Wakati wa kufanya tathmini ya mali makadirio ya fidia hayazingatii kwamba ardhi iliyotolewa itazalisha au la. Na pale ambao kwa makosa ya ukadiriaji mtu akawa amepunjwa; basi hubaki katika lindi la umaskini bila kutarajia. Matatizo kama hayo hutokea kwa kuwa hakuna uwazi katika kufanya biasara ya kuza

ardhi na kusababisha uwezekano wa uvunjifu wa amani na hivyo vyombo vya dola vinapaswa kuwa macho tukitaka amani endelevu, wajumbe walisisitiza.

Baada ya kusikiliza mada na hotuba, washiriki nao waliuliza maswali kwa viongozi wa Serikali kama vile: Je, inakuwaje tunashuhudia ongezeko la migogoro ya ardhi mahali pengi nchini pamoja na kuwepo Sheria za Ardhi? Je matatizo haya yanaashiria kuwepo shinkizo jipya au kuna mahali fulani mambo hayaendi sawa? Je wana jamii wanaufahamu wa kutosha kuhusu sheria hizo au namna ya kuingia mikataba ya ardhi?



# Shukrani kwa kazi ya Injili

Kwa utukufu wa Mungu yalitimia 23 Juni 2013 KKKT ilipofanya Ibada rasmi ya kilele cha Jubilii ya Miaka 50 ya kuundwa kwa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT).

Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Alex Malasusa, aliwashukuru viongozi na wawakilishi wa vyama vya misioni na makanisa toka nje, Serikali na viongozi wastaafu ambao alisema ndio walioweka misingi ili kuhakikisha kuwepo kwa mafanikio na baraka za miaka 50 ya umoja wa KKKT.



Wachungaji waliokuwa katika Ibada ya Kilele cha Jubilii.

## Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani

Katibu Mkuu wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD), Mch. Martin Junge, kwa niaba ya makanisa ya Kilutheri Duniani alipongeza

KKKT kwa kufikia kilele cha jubilii: "Tunafurahi pamoja nanyi, tunawaombea na kuwatia moyo muendeleze wajibu wenu huu," alisema alipotoa salamu.



**Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa, akimsaidia Mch. Junge kupanda mti nje ya maktaba ya Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.**

## Kuelekea miaka 50 ijayo

Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Alex Malasusa, alisema kwa kipindi cha miaka 50 ijayo:

"Kanisa litaimarisha kazi ya kueneza Injili ya wokovu; litafanya utetezi kwa kutoa sauti ya kinabii; litaendeleza kazi za diakonia; litaongeza jitihada za kujitegemea na kuimarisha umoja wa Kanisa.

"Daima tataruka kwa mabawa mawili kama ndege anavyotumia mabawa mawili

kuruka. Kwa bawa moja tutahubiri Injili - yaani maisha ya kiroho na kwa bawa la pili tutafanya kazi za diakonia - yaani huduma kwa jamii.

"Na ndege ambaye bawa moja halipo hawezি kwenda ko kote. Hivyo KKKT tutaendelea kwenda kwa mabawa haya mawili. Tunawashukuru wastaafu kwa kuwa wao walifanya kazi kubwa sana kujenga umoja tulionao sasa."

**Mafuriko Ujerumani:** "Tusiwe watu wa kupohea tu bali pia tuwe watu wa kutoa." Hayo yalismwa na Mkuu wa KKKT alipotangaza ikusanywe sadaka ya pili wakati wa Ibada ya kilele cha Jubilii ya KKKT kwa ajili ya watu waliokumbwa na mafuriko Ujerumani 2013.

## Waziri Mkuu mstaafu awakilisha Serikali

Waziri Mkuu Mstaafu, zingekuwa na Katiba moja tu badala ya kila Dayosisi kuwa na Katiba yake. Alipendekeza mabadiliko ya ajira kwamba mtumishi ye yote wa kanisa ahamishwe kufanya kazi maeneo mengine na si kufanya kazi eneo dayosisi yake iliko.



**Mhe. Dkt. Frederick Sumaye, Waziri Mkuu Mstaafu wa Awamu ya Tatoo (katikati) akifuatiwa na Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa. Kulia ni Naibu Katibu Mkuu Fedha na Utawala KKKT, Bw. Abel Mrema.**  
Picha chini ni baadhi ya Washarika waliohudhuria Ibada ya Jubilii.



## Dkt Dorothea Deneke Stoll

### Mwenyekiti Sinodi Kanisa la Bavaria

Uhusiano wetu na KKKT umekuwa ni wa kusaidiana na kuchukuliana mizigo. Tumeshirikiana kueneza **Habari Njema** na tunaahidi kuwa pamoja kwa siku zijazo. Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Bavaria linasema hongera sana. Kwa kuwa idadi ya wana KKKT 1963 ilikuwa 250,000 na kwa mwaka 2013 inakaribia wanachama milioni saba ni ushahidi wa kazi kubwa iliyofanywa na Kanisa baada ya kupokea mbegu ya Injili toka kwa Wamisionari.

### Mchg. Voller Dally, Mkurugenzi Misioni ya Leipzig

Muziki ni lugha halisi ya mbinguni. Sifa kwa Mungu kupitia muziki inaunganisha dunia na mbingu. Martin Luther alisema muziki unawafanya watu wafurahi, wachangamke, unafukuza mawazo mabaya, unawapooza wanaogombana na hata Shetani anaweza kustahimili. **Kila mwenye pumzi na amsifu Bwana**, Haleluya.

### Askofu Ilse Junkermann

#### Kanisa la Kiinjili Ujerumani Kat

Siku njema huonekana asubuhi. Kweli 19 Juni 1963 ilikuwa siku njema KKKT ilipoundwa kama Kanisa moja. Ilikuwa kweli ni siku njema kwani Wamisionari wa Leipzig walioleta Injili wao ni sehemu ya historia ya kuundwa Kanisa jipya. Nasi tunajivunia kuwa washirika na waanzilishi wa KKKT. Hatujui idadi kamili ya wale waliouwepo katika mchakato huo na kwamba nani alikuwa na maono ya siku njema hii ya leo.

### Mch. Dkt. Fidon Mwombeki,

#### Katibu Mkuu (United Evangelical

#### Mission, Community of Churches in three Continents - UEM)

Kanisa lipanuke lisibaki tu na ushirika wa Ulaya na Marekani kupitia LMC pekee; Lipanue shughuli zake hadi Marekani ya Kusini na Barani Asia.

### Askofu Johannes Friedrich, Muungano

#### wa Makanisa ya Kilutheri Ujerumani

#### Kaskazini (FELCIG)

Tunamshukuru Mungu kwa kuwapo KKKT. Tunamshukuru Mungu kwamba watumbalimbali wameweza kushirikiana pamoja kwa miaka 50 wakisali, kumega mkate na kuhubiri hiyo wakaeneza Injili, wakafundisha, kuponya na kusali. Tufurahi kipekee kwa ushirikiano usio na kifani kati ya Sharika za KKKT na za

# Wasemavyo weng



Ujerumani. Tunaishi nchi tofauti, lugha zetu ni tofauti na mazingira tofauti; lakini tunashirikishana uzoefu ule ule kwa kuwa *sisi tu wamoja katika Kristo. Tumeungana katika Kristo.*

### Mchg. Dkt. Reinhard Kees

#### Berlin Mission Work

Tumetimiza miaka 122 tangu Wamisionari wa Misioni ya Berlin waanze kueneza Injili mwaka 1891 huko Matema ambayo kwa sasa ni Dayosisi ya Konde. Tunavutiwa kuona kanisa halijengi tu **Nyumba za Ibada**, bali inajenga **Kanisa Kuu**; haijengi tu zahanati, bali vituo vikubwa vyaa afya na hospitali kama KCMC na kwamba si shule ndogo zinazojengwa, bali sasa kuna vyuo vikuu kama **Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira**.

### Mchg. Dkt. Klaus Shaffer, Mkurugenzi

#### wa Kituo cha Misioni na Mahusiano

#### ya Ekumene ya Kanisa la Kiinjili la

#### Kilutheri Ujerumani (VELKD)

Nikiangaza hapa tulipo naweza kuielezea KKKT kwamba ni Kanisa lenye sifa kuu tatu: Mwenge unaowaka, nyota na maua. Barani Afrika KKKT ni kama mwenge unaowaka kwa kufanya kazi ya kubeba moto wa Roho Mtakatifu nchini Tanzania na katika nchi jirani na ninaomba Mungu azidi kuwabariki kwa hilo. KKKT ni mionganini mwa makanisa yanayoangaza duniani kama nyota. Naomba Mungu mzidi kuangaza zaidi. Na KKKT ni kama ua linaloeneza harufu nzuri ya **Injili ya upendo wa**



## Neno KUU: Wote waw

**Mungu kupitia Yesu Kristo.** Tunawapongeza na tunawabariki mwendelee kuwa mwenge, nyota na kutoa harufu nzuri kama maua.

### Mchg. Stefan Holmstroem

#### Katibu Mkuu Chama cha Misioni cha Sweden

Nguvu ya msalaba ilitoa msukumo kwa Chama cha Misioni cha Sweden kuanzisha kazi ya Injili Ilula (Kusini mwa Tanzania) na Dongobesh (Kaskazini mwa Tanzania) mwaka 1938. Salamu kwa wana KKKT ni kutoka Wagalatia 6: 14 **"Lakini mimi hasha nisone fahari juu ya kitu cho chote ila msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo."** Msikome kutafuta wanafunzi wapya na vizazi vipyta kwa ajili ya kuwapa ujumbe wa msalaba ambaa ndio pekee unaotuokoa milele. Tunashukuru kwa ushirikiano wa miaka mingi na tungependa kuendelea.

# Jine kuhusu KKKT



## Askofu Mkuu Anders Wejryd Kanisa la Sweden

KKKT imekuwa na mahusiano na Kanisa la Sweden kwa zaidi ya miaka 70. Kwa muda wote huo tumechota baraka nyingi. Ujumbe wangu umefurahi kushiriki kilele cha jubilii ya KKKT. Nawaombea wote walio katika kazi ya misioni waendelee kufanya kazi kwa bidii na kwa uvumilivu na matumaini kwa manufaa ya siku zijazo.

## Mchg. Rune Bucklund Chama cha misioni ya Kilutheri Norway

Hongera sana kwa siku hii. Asanteni kwa ushirikiano katika kazi ya kueneza Injili. Tuliwasaidia ninyi kueneza Injili na ninyi sasa mtaendeleza kazi hiyo. Lakini mtuombee na sisi

tuliopo Ulaya na hasa Norway. Mungu awabariki na asanteni kwa ushirikiano.

## Mchg. Rolf Steffansson Kanisa la Finland

Kwa niaba ya Askofu Gustav Steffansson wa Porvo: *"Furahini nao wanaofurahi;"* Warumi 12: 15. *"Tazama jinsi iliyovo vema na kupendeza, ndugu wakikaa pamoja na kwa umoja,"* Zab. 133. Kwa kushirikiana na KKKT katika kazi hii muhimu ya kueneza Injili baraka zimekuwepo pande zote mbili. (Alikabidhi hundi ya Dola za Kimarekani 1,000 kwa ajili ya vitabu vya theologia katika maktaba Chuoni Makumira).

## Seppo Risanen, Mkurugenzi Chama cha Misioni ya Kilutheri Finland (FELM)

Asante kwa kutoa nafasi kwetu kufanya kazi ya kueneza Injili bega kwa bega nanyi. Tumefanya kazi nyingi lakini kitu cha ndani kabisa ni Injili kuhusu Yesu Kristo ambayo pia inaleta mabadiliko yanayoonekana katika jamii. Na kwa miaka 50 ijayo tuna maono ya kutaka kuwafikishia Injili wale watu ambao bado wako nje ya Kanisa hapa Tanzania na nchi jirani.

## Mch. Mogens Kjaer Katibu Mkuu Danmission

Hongera KKKT. Tunasherehekeea nanyi kwa mafanikio ya kukua kwa kasi kwa KKKT jambo ambalo limekuwa muhimu na la baraka kwa Kanisa la Denmark pia. Chama cha Misioni Denmark kilianza kazi ya kueneza Injili eneo la Bukoba mwaka 1948. Hivyo

tuna historia ya miaka 65 ya ushirikiano na KKKT. Natoa wito KKKT ijenge uhusiano wa karibu na Kanisa la Madagascar.

## Mchg. Carsten Skovgaard-Holm Mkurugenzi wa Misioni Kimataifa Chama cha Misioni cha Kilutheri

### Denmark (DLM) na Naibu Katibu Mkuu

Tumekuwa tukieneza *Habari Njema* kupitia chama Chama cha Misioni cha Kilutheri Denmark (DLM) nchini Tanzania kwa zaidi ya miaka 100. Kazi hiyo tumeifanya kwa furaha na kupokea baraka tele. Ni matumaini yetu tutashirikiana kwa siku zizajo kuwafanya watu wote kuwa wanafunzi wa Yesu Kristo. Tuombe Mungu ili watu wa Denmark, Ulaya na hapa Tanzania wamwamini Yesu Kristo. Hongera kwa jubilii tukikumbuka maneno ya Yesu: *"Nitakuwa nanyi hadi mwisho wa dahari."*

## Askofu Martin Wells Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Marekani

Mimi ni Mmarekani mweusi lakini sjui Kiswahili. Wana-KKKT na watu wa mataifa mengine waliojumuika Makumira; tunaunganishwa kwa damu ya Yesu kupitia mateso, kuwapa wenye njaa chakula, kufurahi na walimwengu na kuwaletaa *Habari Njema* ya furaha kuhusu wokovu. Huko Marekani kuna usemi kwamba 'damu ni nzito kuliko maji'. Ukgombana na ndugu mmoja umegombana na jamaa yake yote. Lakini katika ulimwengu wa Kikristo *maji ni mazito kuliko damu. Maji ya ubatizo yameondoaa utengano wa bahari, lugha ubaguzi wa rangi, umri au umuhimu alionao mhusika.* Alitoa msaada wa Dola za Kimarekani 10,000 kwa Kituo cha Radio Sauti ya Injili ili wazidi kuwafikishia watu Injili kwa njia ya mawimbi.

## Askofu Susan Johnsson Kanisa la Kanada

Nashukuru kwa mwaliko kusherehekeea pamoja na KKKT. Nalitakia Kanisa baraka tele. Nimejifunza mengi katika siku chache za kuwa mionganii mwenu. Kanisa la Kiinjili la Kilutheri la Kanada lina safari ndefu na litajifunza mengi toka KKKT kuhusiana na masuala ya imani na usuhuhuda. Nawashukuru wana-kwaya wote kwa nyimbo nzuri; zimenibariki kiroho na kuimarika kiimani.

# Tu wamoja katika sala na kuhudumiana

Katibu Mkoo wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD) Mch. Martin Junge (pichani) alisema makanisa ya Kilutheri yanatimiza dhamana inayotufanya tuwe wamoja kwa njia ya



sala na kumhurumia jirani.

"Haijalishi sisi ni nani bali ndivyo upendo wa Mungu ulivyo na jinsi atendavyo kazi ili **kutuokoa na kutufanya 'viumbe vipy'a na kutupa maisha mapya**. Na hiki ndicho kiini cha ujumbe wa Injili ya Yesu Kristo akitualika tusizitegemee sana nguvu na jitihada zetu, ila kazi ya Mungu na haki kwa njia ya Yesu Kristo; ili kufikia **maisha yenye uzima tele**."

# Mijuzi ipimwe kwa vigezo vya Biblia

Na Dkt. Msafiri Joseph Mbili

Kwa takribani miongo miili makanisa mengi barani Afrika yameshuhudia waumini wao wakihamia vikundi vya Kipentekoste au Karismatiki. Upentekoste haukazi mafundisho ya msingi ya Imani bali hukaza sana kuhusu matumizi ya karama za Roho Mtakatifu: Kunena kwa lugha na Uponyaji; Mafundisho kuhusu Pepo na nguvu za giza; Ukosefu wa ajira na habari ya Kumtolea Mungu ili akubariki (Utajirisho). Kwa mafundisho haya, viongozi wa vikundi hivi wametajirika kwa kuwa wanamiliki vikundi husika na wana mitandao na vikundi vya ndani na nje ya nchi.

Wanaamini unaweza kujazwa Roho Mtakatifu kama ilivyokea siku ya Pentekoste (Mdo 2: 4). Na huko ndiko 'Kubatizwa kwa Roho Mtakatifu'; na anayebatizwa hivyo anapaswa kupokea uwezo wa kunena kwa lugha na kutenda mijuzi. Wapentekoste hawatoi ufanuzi sahihi wa Mdo 2: 11. Wanaacha ushauri wa Mtume Paulo "Kama mtu akinena kwa lugha, wanene wawili au watatu, si zaidi, tena zamu kwa zamu, na mmoja afasiri", (1Kor 14: 12ff).

Wapentekoste husisitza kwamba watu wengi Afrika na Tanzania wangeweza kuwa na maisha bora zaidi lakini hawafikii hatma hiyo kwa kuwa hawana watu wa kuwaongoza kuiendeza njozi hiyo; na kwamba wapentekoste ndio walioleuliwa na Mungu kutangazia watu wafunguliwe kweli. Neno linalotumiwa: "*Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele*," (Yohana 10: 10).

Tangu uhuru Tanganyika na baadaye Tanzania inapigana vita dhidi ya maadui watatu: *ujinga, umaskini na magonjwa*. Serikali ikishirkiana na mashirika mengine, likiwiemo Kanisa, imejitahidi sana lakini maadui hao bado wapo. Kanisa lina hospitali nyingi, shule na hadi vuyo vikuu. Kanisa linaendesha miradi ya kuondoa umaskini katika jamii.

Baadhi ya wahabiri wa kipentekoste wanadiriki kuwaambia wagonjwa waache kutumia dawa baada ya kuwaombe. Wanasisitiza kwamba Roho Mtakatifu anabadilisha maisha na kuwafanya wawe 'viumbe vipy'a hivyo magonjwa na mikosi itawapata tu 'wale wasioamini'. Mafundisho ya vikundi hivi ni upotoshaji kwa kutumia jina la Injili.

**Mafundisho ya mijuzi yapimwe kwa Neno la Mungu.** Yesu hakupenda kujionyesha wakati akiponya, Yesu hakutumia karama hii ya uponyaji kama njia ya kujipatia fedha wala Yesu hakuponya kwa sehemu bali alimponya mtu na kumsamehe dhambi, (kimwili na kiroho).

Ukifuatilia kwa karibu habari za mijuzi kwa jinsi ya Upentekoste wa kileo, haufuati vigezo vya Biblia. Baadhi ya watu wameanza kushtuka kwani wameona ahadi zao za kuponywa ama kubadilika kimaisha hasa kiuchumi hakutokei na hivyo wanaanza kurudi makanisa yetu.

## Walioshuhudia KKKT ikiundwa



(Kutoka kushoto) Prof. Marja Liisa Swantz toka Finland alisema: "Naleta salamu toka kwa mume wangu ambaye alijenga Luther House. Nimefurahi kuhudhuria shereza za miaka 50 ya KKKT na pia nimefurahi mmo nimekutana na wanafunzi niliowafundisha Shule ya Ashira (Kilimanjaro) kati ya 1952 na 1958."

Mchg. Herb Hafferman ametoka Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Marekani. Alikuwepo miaka 50 iliyopita akifanya kazi KKKT Dayosisi ya Mashariki na Pwani na Seminarini ya Kilutheri Morogoro.

Bw. Johnsson Lutabingwa aliyewahi kuwa Katibu Mkoo KKKT Dayosisi ya Kaskazini Magharibi na Mwenyekiti wa LMC. Alikuwa ni mtumishi Ofisi Kuu ya Kanisa akimsaidia Katibu Mkoo miaka 50 iliyopita.

Mch Horst Becker alitoka Chama cha Misioni Berlin, Ujerumanu. Alisema: "Miaka 50 iliyopita nilishuhudia kuunda kwa KKKT wakati nikiwa Msaидizi wa Askofu, KKKT Dayosisi ya Kaskazini. Sisi sote tumwombwe Mungu na Bwana wetu Yesu Kristo ili siku ile ikifika tuwe pamoa kule mbinguni."

## Kwaya ya Watoto KKKT Dayosisi ya Konde



Kwaya ya Watoto Dayosisi ya Konde ilishiriki matukio ya jubili ya miaka 50 ya umoja wa KKKT. Walikuwa mionganoni mwa wana-kwaya 320 walioshiriki sherehe za jubili.

# Waziri akiri kuwepo kwa ulaghai

Waziri wa Ardhi Nyumba na Makazi ya Watu, Profesa Anna Tibaijuka, alisema kwamba Sheria na Sera za ardhi nchini si rahisi kwa mwekezaji kupora ardhi. Lakini alikubali kwamba ilitokea upungufu mwaka 2001 walipojitokeza wawekezaji wababaishaji waliotumia fursa ya kuwepo msukumo wa kutafuta ardhi ili kulima mibono (jetrofa)

na kusababisha migogoro ya ardhi. Hivyo, alisema, "suala hilo moja lisitumike kufanya watu waamini kijumla kwamba uwekezaji ni jambo baya".

Katika mkutano huo Prof. Tibaijuka alitoa mada: "*Serikali Inavyoijihusisha Kuzuia Migogoro katika Biashara na Utoaji wa Ardhi nchini*" na ndiye aliyefunga

mkutano huo kwa niaba ya Waziri Mkuu.

Prof. Tibaijuka alisababisha baadhi ya wajumbe kutoelewana baada ya kutamka: "*Ufugaji wa asili hauna nafasi kubwa ya maendeleo ya kiuchumi nchini kwa sasa.*" Na kuongeza kusema kuwa maeneo mengi duniani watu wanaachana na kazi ya kilimo (na ufugaji

na kuhamia sekta nyingine ili kutoa fursa ya uwekezaji mkubwa katika sekta ya kilimo na mifugo.

*"Tuache kujidanganya kwa kuishi tulivyozoea kwa kung'ang'ania ardhi tusiyo-weza kuitumia. Ni sawa na chura ndani ya dimbiwi anayesema 'maji yangu', 'maji yangu', kumbe hawezikunywa yote akayamaliza,"* alisema.

Kuhusu rushwa, Waziri alitoa changamoto kwamba viongozi wa dini wakazanii mafunzo kuhusu maadili mema kwa waumini wao ili kuondoa dhuluma na matumizi mabaya ya madaraka. Pia alitoa changamoto kwamba haki katika ugawaji na matumizi ya ardhi ianze ngazi ya familia.

Mhe. Benjamin William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu akitoa mada kuu alisema: Watu wanaodhani kwamba upo uporaji wa ardhi wamepotoshwa na kwamba jambo kubwa lililo wazi ni kwamba ardhi iliyopo nchini hajatumika kwa kiwango cha kutosha.

Alisema njia nzuri zaidi ya kupata maendeleo ni kwa uwekezaji mkubwa na kuendesha kilimo na ufugaji wa kisasa na kukuza uzalishaji ili wote waweweze kunufaika.



Muda mfupi kabla Waziri Mkuu hajafungua mkutano huo Kwaya ya Watoto ya Shule ya Jumapili ya Usharika wa Msasani, jijini Dar es Salaam, iliimba wimbo uitwao: 'Mkutano wa Dharura' uliowaangaliza viongozi kuwa macho na masuala ya ardhi ili pawe na amani endelevu na nchi yetu isirudi utumwani.



Viongozi wa Serikali katika picha ya pamoja na Kamati ya Maandalizi ya Mkutano wa "Haki Ardhi kwa Amani Endelevu." Walioketi kutoka kushoto Waziri wa Ardhi, Prof. Tibaijuka, Rais Mstaafu Mhe. Benjamin Mkapa, Waziri Mkuu Mhe. Mizengo Peter Pinda, Mwenyekiti wa Mkutano, Askofu Dkt. Munga na Mkuu KKKT Dayosisi ya Konde, Askofu Dkt. Israel-Peter Mwakyolile.

# Wajibu wa Kanisa kukabili mafundisho potofu

Na Mch. Dkt. Faith K Lugazia

Kukabiliana na mafundisho potofu ya vikundi ya Kipentekoste ambavyo hutumia vibaya vifungu ya Biblia ili kuvuta wafuasi; ninasihi viongozi wa Kanisa tuweke mkazo wa kufundisha. Tufundisho nini? Tuwe na utaratibu wa makusudi wa Masomo ya Biblia ili waumini wetu wafahamu tofauti ya mafundisho yetu na upentekoste wa kileo.

Mafundisho yao yanafanana na ya kwetu lakini yakiwa na maana tofauti. Wao wanaamini kuna aina tatu za ubatizo na katika hizo zote 'hakuna Sakramenti'. Muumini anaanza kwa kuokoka (kujihesabia haki). Ubatizo huja baadaye akimaanisha haya: Aina ya kwanza ya ubatizo ni ule wa toba (Mdo. 19: 4) - wa Yohana Mbatizaji ambaa hauhitaji maji ila ni alama inayokufanya kuwa sehemu ya mwili wa Kristo wakati wa kuokoka. Ubatizo huu una maana mbili: Kwanza unakufanya wewe ujiunge na familia ya Mungu (1Kor 12: 13). Kwa ubatizo huu mtu anakuwa 'amezaliwa mara ya pili' na hapo anageuzwa (Warumi 12: 1 – 2). Pili ni ubatizo wa Roho Mtakatifu ambapo hapo unapokea karama ya kunena kwa lugha na matendo mengine ya miujiza. Waumini wetu wakifahamishwa haya, wataona ubatizo mwininge wo wote hauna maana kama si Sakramenti.

'Injili ya Utajiri' ni mafundisho kwamba ukimwamini Yesu na ukaamini ahadi zake basi utabarikiwa na kukua kiroho, kimwili (afya)



Mch. Dkt. Lugazia

na utatajirika. Hueleza kuwa umaskini si mapenzi ya Mungu bali ni alama ya dhambi ama kukosa Imani, (Kumb 28: 3 - 13). Vifungu vinaelezea Bwana alipowaambia wana wa Israeli *wachague uzima ili baraka zote zilizotajwa ziwe juu yao*. Hivyo, utajiri wa fedha na afya njema pia ulitolewa na Mungu mwenyewe wakati wa kutupatanisha, mafundisho ya kinukuru (2Kor 8: 9). Pia Mfundisho ya 3Yoh 2. Mafundisho haya hukaza kuwa watu wanahitaji kupanda mbegu yaani kutoa sadaka kubwa ili baadaye waje wavune mavuno mengi. Usahihi ni kwamba Paulo na Yohana wanazungumzia utajiri wa kimwili na kiroho lakini wana-vikundi hivi wanakaza utajiri wa kidunia. Hapa kwetu tukaze utajiri lakini tukifundisha kuwa: Hatutoi ili tupate. Wala hatutoi kwa sababu tumepata mali na utajiri. Tunatoa kwa sababu tunamshukuru Mungu kwa kazi kubwa aliyoifanya msalabani ya kutukomboa; kutufanya wema na kutupa vipawa vyote tulivyonavyo.

Ili kukabili Upentekoste wa kileo na vikundi ya Karismatiki pia, tukaze kuwa usomaji wa Biblia pekee, kiroho hautoshi; ubatizo usio wa Sakramenti si shahidi kwani unalenga mtu kujihesabia haki; tusikubali kupotosha mafundisho kuhusu kuokoka na kupanga

karama anazotoa Roho Mtakatifu katika daraja za umuhimu (kwamba kunena kwa lugha, uponyaji na matendo ya miujiza ni muhimu kuliko karama nyingine). Iko haja kwa kanisa kuweka umuhimu katika kufundisha na kuongoza. Mafundisho kuhusu Roho Mtakatifu na madhumuni ya karama atoazo Roho Mtakatifu vinapaswa kufundisha katika upana wake inavyostahili.

**Kanisa linapaswa kuhudumia watu wanaosumbuliwa na nguvu na mamlaka za dunia hii.** Tuanzishe vituo ya huduma ya maombezi na kuwapanga Wachungaji wenye karama kwenye vituo hivyo wakisaidiana na waumini raia wenye karama. Na Kanisa liunde jopo la watheologia wasomi wakisaidia muelekeo wa Kanisa katika kukabiliana na changamoto zilizo mbele yake. Wajibu wa kanisa si kuwapa waumini kila kitu wanachotaka bali wapewe kitu wanachotitaji. Kwa kutoa huduma za maombi na maombezi ya uponyaji kwa waumini Kanisa letu litakuwa limetoa huduma ambayo ni hitaji.

## MAONI YA MSOMAJI Kiburi huzuia mafanikio

*Ndugu Mhariri*

Napenda kuchangia maoni yangu kuhusu kiburi. Kiburi ni ile hali ya mtu kujiona yeeye anafaa kuliko wengine na hivyo kujikweza. Kiburi ndio mzizi na asili ya dhambi zote. Na kiburi ndio dhambi iyooneea kuliko dhambi zote kwani dhambi zote hutokana na kiburi. Haya yote hutokea pale mtu anaposikia sauti ya Mungu na kukaidi, na matokeo yake huishia katika uangamivu. Wazazi wetu Adamu na Hawa walipokaidi sauti ya Mungu waliishiua kuangamia (Mwanzo 3). Kanisa na Taifa kwa ujumla linatakiwa liwe na watu wenye hofu ya Mungu. wanyenyekevu na wenye kutii sauti ya Mungu. Kiburi cha mafanikio na ubinafsi ndivyo vinavyosababisha Kanisa la Mungu kuyumba kote ulimwenguni. Watu kupenda mafanikio ya haraka na kutukuzwa vimesababisha watu kuasi sauti ya Mungu (kiburi).

Mataifa yanaingia katika migogoro kutokana na viongozi kuwa wakaidi na wasiojali sauti ya Mungu na hivyo kuondolewa utukufu. Kiburi ndicho huondo utukufu wa mtu, (Danieli 5:20, Isaya 14:12-20). Nebukadreza aliondolewa utukufu kwa sababu ya kiburi. Hata kama ungefanya jambo zuri sana kiasi gani lakini kukiwa na hali ya kudharau wengine maana yake hupotea. "Ee Mungu ninakushukuru kwa kuwa mimi si kama watu wengine, natoa zaka mera mbili kwa juma, nafunga na kutoa zaka". Hapa tatozo ni mimi si kama watu wengine.

Kanisa halitaweza kuendelea lisipokuwa na watu wanyenyekevu, wanaofundisha unyenyekevu na wenye kuishi kwa unyenyekevu. Na Kanisa likikosa watu hao basi na Taifa litawakosa, kwani Kanisa ndio chimbuko la viongozi. Taifa la Israeli lilipokuwa na viongozi wanyenyekevu ilifanikiwa, lakini walipokuja viongozi wasio na hofu ya Mungu liliingia matatizoni na kisha likagawanyika.

Kwa hiyo, kiburi kinawenza kutugawa kama Kanisa na kama Watanzania. Hivyo sisi kama Kanisa la Mungu ni lazima tuwe watu wa mfano badala ya kukaa kimya, kwani tunayo mamlaka makubwa sana. "Ninyi ni nuru ya Ulimwengu." Kwa hiyo ni lazima tuchukue hatua.

Mwj. Samwel Kasigwa Kayanda  
K.K.K.T Usharika wa Mwisenge, Musoma  
Simu 0755 787 360, 0787 787 360  
E-mail: [yangadasamwel@yahoo.com](mailto:yangadasamwel@yahoo.com)

## Kukosekana maadili taifa linaenda pabaya

Na Mch. Dkt. Stephen S. Kimondo

Siku za karibuni tumeshuhudia wimbi la vitendo viovu hapa nchini. Mionganini mwa matukio hayo ni mauaji ya viongozi wa dini; mauaji ya mwandishi wa habari David Mwangosi; kutekwa na kuteswa kinyama kwa akina Dkt. Steven Ulimboka, Mwenyekiti wa Jumuuya ya Madaktari, Absalom Kibanda Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri, nk.

Arusha tumeshudia milipuko ya mabomu kanisani na kwenye mikusanyiko ya watu, ambapo watu wasio na hatia walipoteza maisha. Vitendo hivi ni uvunjwaji wa dhahiri wa "Amri ya Tano" inayokataza kuua.

Katika mazingira ya jinsi hii vyuo vikuu nya Kanisa na vingine vinapaswa kuwafundisha wanafunzi wao "Somo la Misingi ya Imani na Maadili" ili watambue umuhimu wa kuthamini uhai wao na wa wengine.

Kozi hiyo, ihmize wakati wote kufanya maamuzi sahihi kuhusu maisha yao binafsi na kujiepusha na vitendo vinavyoweza kuleta madhara, maafa, au majuto kwao binafsi na kwa watu wengine.

Somo la maadili liwaandae wanafunzi kuwa viongozi bora wenye wajibu wa kuifanya Tanzania na Afrika kwa jumla pawe mahali salama kwa watu kuishi kwa upendo, amani, utulivu, na mshikamano wa kindungu.

Somo likifundishwa vizuri litasaidia kuundwa kwa jeshi la kuleta chachu ya mabadiliko yenyne neema na baraka kwa

taifa. Kama wanafunzi wakizingatia maudhui ya somo hili, hakika Tanzania itakuwa mahali bora kwa makazi ya watu na mahali ambapo "maisha bora kwa kila Mtanzania" yatawezekana.

Na jamii katika ujumla wake ina wajibu wake katika malezi ya vijana wetu kimaadili.

Watu wote, kila mmoja mahali alipo, na kwa ngazi yake, ashiriki kwa tabia na mwenendo wake kuwaelekeza vijana kuwa na maadili mema. Kila mmoja wetu anao wajibu katika malezi ya kimaadili kwa vijana wetu.

Kila mmoja wetu anapaswa kuwa mfano ulio bora wa maisha ya kimaadili kwa vijana. Maisha ya viongozi wa Kanisa katika ngazi zote kuanzia kwenye Mitaa, Sharika, Jimbo, Dayosisi, na Kanisa ngazi ya taifa, lazima yawe ya mfano kwa vijana wetu.

Namma tunavyoishi, kauli zetu na vitendo, vyetu ni lazima vilingane na mafundisho ya Neno la Mungu. Mahali pengi viongozi wa Kanisa wanatazamwa kama kielelezo cha maisha sahihi ya kimaadili, na hivyo kutazamiwa kuwa na maisha ya mfano wa kuigwa.

Jamii ikishiriki wajibu huu, Tanzania itakuwa mahali bora ambapo watu wanahishi kwa pamoa kwa upendo na ambapo viongozi wanatumia madaraka yao kwa faida ya raia ili raia wafaidi matunda ya maliasili ambazo Mungu amezitoa kwa Watanzania.

# Wakati umefika Sharika kusaidiana

Na Mch. Prof. Wilson Niwagila  
Josiah Kibira University College

## Misioni ya ndani

Kanisa linahudumia waumini wakue kiroho na Imani iwe thabiti. Ni mahali pa kuhamasisha waumini wafahamu wajibu wao kama wafuasi waaminifu wa Bwana Yesu, wakihudumiana na kuhudumia watu wengine.

Sharika zetu zinatofautiana kitakwimu, kimaendeleo na kimapato. Kuna sharika tajiri na sharika maskini lakini sharika tajiri hazisikii deni kusaidia sharika maskini. Hapa kuna hali ya kusahau tulikotoka. Mwanzoni hata sharika tajiri zilikuwa katika hali ya umaskini ndipo vyama vya misioni vilikusanya fedha toka sharika na wakristo wenye moyo wa kuhudumia watu wa nchi nyingine.

Sasa hapa kwetu Tanzania sharika tajiri zinafanya mambo mengi yenye gharama kubwa lakini hazitupii macho kuona sharika zenyenye mahitaji ya msingi.

Dhambi kubwa ya kutajirika, ni kutokuwa na nidhamu ya kutumia utajiri kwa manufaa ya maskini. Ubinafsi ni tunda la uchoyo. Ikiwa sharika tajiri haziwezi kutambua hili basi tujue kwamba ndio mwisho wa kukua kiroho.

Misioni ya ndani inapaswa kuwa na macho kuona mahitaji ya watu wa Mungu. Inapaswa kuwa na masikio kusikia kilio cha uumbaji wa Mungu. Inapaswa kuwa na miguu kuondoka pale ilipo na kufika penye tukio. Inapaswa kuwa na mikono kutenda yale yote yaipasayo.

Kitabucha Kutoka 3:7-10 nichangamoto kwa kanisa kuelewa maana ya misioni ya ndani na nje. Kanisa haliwezi kufaulu kama halifiati sera ya Mungu: KUSIKIA vilio vya watu wa Mungu; KUONA dhuluma, uonevu na mateso ya uumbaji wa Mungu; KUONDOKA na kuelekea kwenye matukio na KUWAJIBIKA kwa njia yo yote ile ili watu wa Mungu na uumbaji wake ufurahie UKOMBOZI wa Mungu.

## Misioni ya Nje

# Wakristo yapimeni mawazo ya utandawazi - wito

Na Prof. Wilfred Mlay,  
"The Great Lakes Initiative  
Leadership Institute on Peace  
and Reconciliation".

Miongoni mwa mambo chanya ya utandawazi ni kwamba makanisa ya nchi zinazoendelea yanashiriki kutoa michango yao ya hali na mali na yana mguso kimataifa. Kanisa letu baada ya kupokeea Injili toka kwa Wamisionari likafanya misioni ndani na nje ya nchi.

Utandawazi umeleta mambo ya manufaa na mambo yanayotoa changamoto kwa jamii na makanisa

Mch. Prof.  
Wilson  
Niwagila.



Hapa yanaweza kuwa maeneo ya kijografia tulivyozoea, kwa kuanzisha maeneo mapya. Pamoja na hayo maeneo mapya yana maanisha pia kukabiliana na changamoto mpya ambazo hatukuzoea, kwa mfano mfumo mpya wa mawasiliano, lugha mpya, uhusiano kati ya wasomi na watu amba si wasomi, uhusiano kati ya matajiri na maskini, uhusiano kati ya vyama vya siasa vikiwa na lengo moja la kumhudumia mwananchi bila kupoteza muda mwinge kwa malumbano. Matabaka haya yote yako ndani ya usharika. Mchungaji au Mwinjilisti atafauluje kuwahudumia hawa wote wajisikie kwamba ni familia moja katika usharika na katika taifa?

Kanisa linakabiliwa na changamoto

kubwa katika kueneza Injili kwa miaka 50 iliyo mbele yetu. Ni dhahiri kwamba changamoto hizi zinaendana na mabadiliko makubwa na ya kasi kwa mujibu wa uvumbuzi mpya wa mambo ya sayansi, utandawazi, mabadiliko ya tabia ya nchi, tamaduni na mapokeo. Kanisa haliwezi kuzuia mabadiliko haya lakini lazima liwe makini katika kukabiliana na changamoto hizi. Kanisa lina sura mbili kama shilingi; upande mmoja Kanisa limepeewa mamlaka ya kufundisha, na upande wa pili Kanisa limeambiwa kwamba ni Mwanachuo.

Roho wa Mungu yupo ndani ya Kanisa akielekeza, akiongoza na kufundisha ili kukabiliana na mabadiliko pamoja na changamoto zake. Kuwa mwana chuo ni kusikiliza mwalimu, kufanya kazi za mwalimu, kufanya utafiti ili kubaini mambo muhimu yatakayomsaidia kuwa mwanachuo mahiri wa kuelekezawengine katika kufaulu mitihani ya maisha. Hapa napenda kusisitiza kwamba maendeleo mazuri ya mwanachuo ni kutopoteza muda alionao, tena ni kubaini kila msaada uliopo kuijendezeza. Bahati nzuri siku hizi mtu unaweza, ukitaka, kujifunza mambo mengi yenye manufaa; kwa njia ya mitandao popote pale. Huna haja ya kwenda maktaba iliyo mbali.



Prof.  
Wilfred  
Mlay



pia. Lakini athari mbaya za utandawazi ni pamoja na ongezeko la kundi la watu walio na umaskini uliokithiri; uharibifu wa mazingira; vita na migogoro kila mahali; ubepari kushika mizizi na hali ya watu kupenda kutajirika.

Utafutaji wa malighafi, hasa mazao na rasilimali nyingine, kwa ajili ya viwanda

katika nchi tajiri; unaleta uharibifu wa urithi wa asili kwa manufaa ya walio matajiri.

Katika utandawazi mawasiliano yameboreshwa hivyo kurahisisha mahusiano ya karibu baina ya mataifa; kati ya mtu na mtu au baina ya makundi yakiwemo madhehebu au vikundi katika taifa na kimataifa.

Kuna watu wanaoga mambo mageni wanayoona, kusikia au kusoma kuititia vyombo vya mawasiliano. Kwa mfano kuna wanaohubiri Injili ya Utajirisho – kwamba utee sadaka uwe tajiri kama vile Biblia inaruhusu tamaa ya mali.

Ili kukabiliana na utandawazi, Kanisa linatakiwa liishi Injili kwa kuiga kilichofanywa na kanisa la mwanzo lililofanya kanisa liwe ni mahali pa makimbilio na matumaini.

# Siku ya Bwana 23 Juni 2013, ilikuwa njema sana. Viongozi wa Kanisa wa ndani na nje ya Tanzania walihudhuria Ibada ya kilele cha Jubilii ya miaka 50 ya umoja wa KKKT Chuoni Makumira.



## Mauaji ya Vikongwe

Kanisa limeahidi kuingilia kati vita dhidi ya mauaji ya vikongwe katika Ukanda wa Ziwa. Ahadi hiyo ilitolewa Shinyanga na Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Alex Malasusa, 24 Nov. 2013 katika Ibada ya kuweka wakfu Kanisa Kuu la Usharika wa Ebenezer, KKKT Dayosisi Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Bibi Annarose Nyamubi, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga; aliomba Kanisa lisaidie kunusuru maisha ya vikongwe wanaouawa na ndugu zao bila hatia yo yote kwa imani za kishirikina. Alisema: "Hapa Shinyanga tumechoka kusikia habari za mauaji ya vikongwe; hivyo naomba Kanisa lisaidie kwa kufikisha Injili vijijini."

## Kanisa halitakwepa utandawazi

Na Mchg. Dkt. Elieshi Mungure Katibu wa Afrika wa FMKD

Kanisa haliwezi kukwepa mguso wa utandawazi maana '*lipo ulimwenguni, ingawa si la ulimwengu.*' Kanisa kama jamii ya walio itwa na kutumwa na Kristo kwa nguvu ya Roho Mtakatifu; lina uhai, linaendelea, linakua na lina nguvu ya pekee ya Roho Mtakatifu.

Kanisa letu Afrika linajihuisha na Misioni ya Mungu katika ulimwengu, linatoa huduma ya diakonia, elimu na mafunzo ya theology, linafanya utetezi na huduma nydingine. Lina watu nje na watu wa nje wako hapa.

Kanisa la Kilutheri Afrika lina makanisa 31 yenye wakristo karibu milioni 20. KKKT 2013 ilikuwa na waumini milioni 6.1. Mchangwo wetu ni mkubwa na una mguso ulimwenguni kote.

Akijadili mada kuhusu "Utandawazi" alisema Kanisa linahusika kufanya utetezi kwa kina kutokana na viashiria na matokeo ya maadili mabaya yanayochangia ukosefu wa amani, matumizi mabaya ya mali ya umma kama ardhii na rasilimali nydingine. Kutokana na haya inabidi kanisa lifanye utetezi wa maadili mema na kutenda haki. Pia kanisa na wana-kanisa wanategemewa wawe mfano wa maadili mema katika jamii.

Katika utandawazi kumekuwa na ongezeko la mahusiano ya karibu na imani zingine bila maandalizi. Barani Afrika tuna mifano ya vikundi nya kiimani venye mafundisho ya 'uamsho' uliopilitiza. Matokeo yake ni kusababisha vurugu. Kuna vikundi nya Boko Haram, Nigeria na Al-Shabaab Afrika Mashariki. Kanisa litumie nafasi yake ya unabii ili kujenga mazingira

Mchg. Dkt.  
Elieshi Mungure  
Katibu wa Afrika  
wa FMKD



ya amani na kusimamia haki hata pamoja na kuwepo makundi ya imani tofauti na sisi.

Hivyo, Kanisa livikumbushe vyombo nya dola kuchukua nafasi yake kwa kuhakikisha vinasimamia haki na amani kwa watu wote.

Ni wajibu wa vyuo nya theology nya KKKT kukuza mafundisho yanayoelekeza namna ambayo watu wote wanawea kuishi kwa amani na kuwa na mahusiano mema licha ya tofauti zao (peaceful co-existence).

Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD) limeanzisha mitandao katika mabara yote saba duniani. Na mara baada ya Kongamano la Theoloja liilofanyika Witternberg, Ujeruman, Oktoba 2012; wanachama wa FMKD walikubaliana kuimarisha elimu ya theology katika vyuo kwa kuimarisha mahusiano kuitia mitandao.

Lengo ni kutumia nafasi ya utandawazi kwa kuanzisha mitandao ya mawasiliano kusaidia kuimarishana katika mitaala na jinsi ya kuandaa mada au mafundisho yagusayo masuala ya kila siku. Lengo jingine ni kumegeana vipawa kwa kuhamasisha tabia ya kuandika maandiko yanayogusa mambo mapya.

**WAJIBIKA**  
Juma la Mazingira  
KKKT ni 3 - 9 Machi  
kila mwaka.

## Miaka 100 ya Injili Ulanga -Kilombero



**Askofu Reinhard Mtenji,  
KKKT Dayosisi ya Ulanga- Kilombero.**

Pamoja na kwamba Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) limetimiza miaka 50 ya umoja tangu makanisa saba yaliyoanzishwa na Wamisionari kuungana; Injili kuitia Kanisa la Kilutheri iliingia nchini miaka 126 iliyopita. Ndiyo sababu kwa wakati tofauti Dayosisi za KKKT zimeadhimisha Ibada ya miaka 100 tangu Injili iingie eneo husika. Kwa mfano 1-2 Agosti 2013 KKKT Dayosisi ya Ulanga- Kilombero ilisherehekea jubilii ya miaka 100 mjini Ifakara. Kituo cha kwanza cha misioni kilianzishwa Lwamate Forest Tanganyika Masagati na Mmisionari wa Kijerumani, Dkt. Alexander Merensky, toka Chama cha Misioni cha Berlin 1908.

## Ujumbe wa Danmission watembelea KKKT



Picha ya pamoja ya menejimenti ya KKKT na ujumbe wa Danmission ulifika Ofisi Kuu ya KKKT mwezi Novemba 2013 ukiongozwa na Mch. Mogens Kjaer, Katibu Mkuu Danmission; ujumbe huo ulipokuwa njiani kuelekea KKKT Dayosisi Mashariki ya Ziwa Victoria. Walioketi wa tatu kulia ni Naibu Katibu Mkuu Fedha na Utawala, Bw. Abel Mrema aliyekuwa kaimu Katibu Mkuu.

# Nyakahanga kujenga chuo cha uganga

Kwa kutambua maendeleo yaliyopatikana tangu kuanzishwa mwaka 1912, Hospitali Teule ya Nyakahanga ya KKKT Dayosisi ya Karagwe, imepanga kuanzisha Chuo cha Uganga.

Hospitali hiyo imetoa mchango mkubwa wa huduma za afya nchini na hasa kwajamii ya wana-Karagwe kwani hospitali hiyo Teule inatoa huduma kwa miaka 100 bila ubaguzi. Mafanikio mengi yanaonekana: kwa mfano wakati wa maadhimisho ya jubilii ya miaka 100 ya hospitali hiyo, hivi karibuni, yalikuwepo maonyesho ya historia ya hospitali; warsha za huduma na elimu ya afya; pia hazikukosekana burdani. Kwa kuwa msisitizo ulikuwa ni huduma za afya; madaktari wa hapa na kutoka nje walijumuika kuchunguza afya na kutoa ushauri kwa watu mbalimbali waliojitekeza.

Hospitali ya Nyakahanga ilianza kwa kutoa huduma kama zahanati ndogo tu ilioanzishwa na Wamisionari wa Kijerumani. Na haukupita muda mrefu kazi ya kituo iliendelea kupanuka hadi 1963 kituo kiliweza kupandishwa hadhi na kuwa hospitali.

Kwa muda wote huu tangu 1912 hadi sasa wafanyakazi wa afya, madaktari na wauguzi wanafanya kazi kwa juhudni

kubwa, ufanisi, ujuzi na maarifa ili kutoa huduma ya kiwango cha juu kwa wagonjwa wanaowahudumia.

Kwa ushirikiano na washirika na wadau mbalimbali hospitali imeweza kufunga vifaa tiba vya hali ya juu na vya kisasa. Na wakati wa kusherehekeea miaka 100 ya Hospitali ya Nyakahanga walikuwepo watu toka ndani na wawakilishi wa washirika wa kutoka nje ya nchi.

Siku hiyo walijumuika katika sherehe walikuwa ni pamoja na wawakilishi wa Serikali, wafadhili, mashirika yasiyo ya kiserikali, taasisi za Kanisa, taasisi za imani, asasi za kiekumene, mashirika ya kiserikali, wamisionari, watu wanaofanya kazi kwa kujitolea na makampuni binafsi.

## KKKT inaandaa Sera ya utoshelevu wa chakula

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) limetoa rasimu ya kwanza ya Sera ya Chakula. Kanisa limetoa rasimu hiyo kama mdau wa maendeleo nchini na kama mchango wake kufanikisha ‘Dira ya Taifa 2025.’

Naibu Katibu Mkuu Mipango na Maendeleo KKKT, Bw. M. W. Mallumbo, alisema hivi karibuni kwamba ili Kanisa lifanikiwe kutimiza dhamira ya kuinua hali ya maisha ya watu kiroho, kimwili na kiakili, limeona lisaidie pia ili watu wawe na uhakika wa chakula chenyehirutubisho vinavyohitajika mwilini. “Chakula kikiwepo katika ngazi zote kuanzia kaya hadi taifa ndipo unapoweza kuzungumzia kuhusu ‘uhakika wa chakula,’ alisema.

Lengo la Sera ya Chakula KKKT ni kusaidia kuboresha mfumo na kuhamasisha ushirikishwaji wa wananchi wakati wa kubuni, kupanga na kutekeleza mipango ya kuzalisha na kuhifadhi chakula. Hiyo itakuwa ni namna bora ya kuwa na utoshelevu wa chakula bora wakati wote kuanzia ngazi ya kaya.

# Wote wawe na umoja

**Yoh 17: 21**



Baadhi ya viongozi wa Kanisa wakati wa kuweka jiwe la msingi jengo la Nyaraka za Historia za KKKT linalotarajiwa kujengwa katika Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.

**Na Askofu Dkt. Samson Mushemba,  
Mkuu Mstaafu, KKKT**

Makanisa saba ya Kilutheri yaliyokuwa yameanzishwa na Wamisionari wa Ulaya na Marekani nchini Tanganyika mnamo 19 Juni 1963, yaliungana na kuunda Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanganyika (KKKT) na baadaye Tanzania. Kabla ya hapo makanisa hayo ya lihusiana kama fungamano; lakini yalipoungana yalikubaliana kuwa na Katiba moja iliyoanzisha KKKT.

Kanisa hili ni kiungo kimoja cha Yesu Kristo katika dunia nzima. Limejengwa katika misingi ya mahubiri ya manabii na mitume kama kanisa la kwanza. Kanisa la kwanza lilifanya yafuatayo ili kudumisha umoja:

Kwanza lilidumu katika mafundisho ya mitume yaliyojengwa katika Neno la Mungu. Viongozi wa kisiasa nchini wamekuwa wakitukumbusha umuhimu wa kukaa katika misingi ya umoja wetu kama taifa. Tunafahamu ‘umoja ni nguvu.’ Neno la Mungu ndilo lilobeba umoja na yote Mungu apendayo tuyafahamu.

Kanisa la kwanza pia lilidumu katika kusikiliza na kujunza Neno. Mwongozo na maoni mazuri ya wachamungu yanatokana na Neno la Mungu. Washarika wanaotaka kuongozwa na kukaa katika uzima husoma Neno la Mungu kila siku wakilitafakari na linakuwa ‘chakula’ chao cha kila siku. Wanalisikiliza katika Ibada, mikutano ya kiroho, nk. Mfalme Daudi alisema katika Zaburi “Neno lako ni taa ya miguu yangu na mwanga wa njia yangu”.

KKKT tunapokumbuka miaka 50 ya umoja; tupende kusikiliza na kulitafakari Neno la Mungu ambalo ndilo ‘linaloweza kuonya na kuwabadilisha watu hasa watenda mabaya na kuwafanya wawe watu wa Mungu.’ Neno linaweza kuwabadilisha wala rushwa, wauaji, wanaochukia wenza, wanaouza miili yao na walio na ubinasi kiasi cha kuharibu mazingira yetu, nk. Linaweza kuwabadiishi wabadirifu wa fedha za umma katika manispaa au halmashauri, nk. “Apendaye Neno la Mungu atakamilishwa aweze kutenda kila tendo jema,” kama Paulo

asemavyo.

Kanisa la kwanza lilidumu likimshuhudia Yesu Kristo aliyeagiza: “Nanyi mtakuwa mashahidi wangu kuanzia Yerusalem, Uyahudi yote, Galilaya na hata mwisho wa dunia.” Hivyo kanisa la kwanza kwa umoja, lilimshuhudia Kristo. Mahubiri yakifuatana na uchaji; huvuta wengine wamjje Kristo na kumwamini.

Kanisa la kwanza lilifuata maagizo ya Yesu kwa kudumu katika kumwomba Mungu. Maombi yanamuunganisha Mkristo na Mungu. Na Mungu anasikia na kujibu sala za watu wake waombapo katika jina la Yesu. Bwana Yesu alisema: “Ombeni nanyi mtapewa, bisheni nanyi mtafunguliwa.”

Katika umoja kanisa la kwanza waliomba na walikumbuka jinsi Bwana Yesu Kristo aliviyokuwa akiomba. Kuna siku aliomba usiku kucha alipotaka kuchagua mitume na pale alipokaribia kuteswa. Mitume walisinzia lakini Yesu akaendelea kuomba na aliporudi aliwaliza “mbona mmesinzia?” Kuomba ni msingi wa uhusiano wetu na Bwana Wetu Yesu Kristo. Yesu alimwombwa Mungu sana na sisi inatupasa tumwombe Mungu. Nawasihi tunapoingia kipindi hiki cha miaka mingine 50 ya umoja wa KKKT; tuingie katika kuomba hadi Yesu atakaporudi. Tuombe Mungu atupe amani,

Askofu Dkt. Samson  
Mushemba akihubiri  
wakati wa kilele cha  
Jubili ya KKKT.

atuondolee chuki, uadui na uhassama; si katika Kanisa tu; bali katika makanisa mengine pia. Tuombe watu wamjue Mungu na kumpenda na kumwamini Yesu Kristo aliye mkombozi wa dunia. Wakristo wakimwomba Mungu kwa imani atawasikia na kujibu sala zao. Petro alipofungwa (Mdo 12: 5 -11); Mungu alitumia malaika wake pingi zikalegea, milano ikafunguka, Petro akatoka na alipofika chumba walimokuwamo wenzake; aliwakuta wakimwombea. Tuliombee taifa letu, watoto na jamaa zetu na tuombe umoja udumu katika Kanisa letu ili “Mungu azidishe watu wanaookolewa.” Neno la Mungu linasema “bali wote waliompokea Bwana Yesu alipapa uwezo wa kufanya watoto wa Mungu,” na hao ndio wale waliaminilo jina lake. Wokovu wetu umetokana na Mungu kwa njia ya Yesu Kristo.

Kanisa la nyakati za mitume liliwuwa likimsikia Bwana Yesu akiliombea, akifundisha, nk. Kanisa hilo liliumbana na mateso na upinzani sana katika siku za mwanzo kutoka kwa watawala na viongozi wa dini na Wayahudi; lakini halikukata tamaa. Lilidumu katika kumpenda Bwana Yesu, likimtangaza na kumshuhudia; na Yeye akalimarischa likashinda. Na likawa ndio chimbuko la misioni iliyotumwa “ulimwenguni kote” kuanzia Uyahudi, Ulaya, Afrika, Asia, nk. Maombi yao yaliambatana na ushirika, kuumega mkate na kumshudia Yesu Kristo kwa nguvu na katika umoja. Na watu waliokolewa na kuijunga na kanisa. Basi ndani ya kanisa hilo Mungu akatenda maajabu makubwa na kanisa hilo linadumu mpaka sasa.

KKKT limerithi yaliyofanya na kanisa la kwanza na maisha yake kwa sababu hayo ndio yanayolifanya kuwa kanisa lenye umoja na lisilo na mwisho. Utumishi na maisha ya Kanisa la Kilutheri uige mfano wa kanisa la kwanza lilioanzishwa na mitume; na ndivyo tunavyotaka iwe po pote duniani.

Mungu abariki KKKT ili liendelee kujenga utumishi na maisha yake katika msingi ulioanzishwa na Yesu. Na likifanya hivyo, litazidi kufanikiwa, kubarikiwa, kuimarka na kuweka wakristo na wafuasi wake wote katika njia iendayo kwa Bwana Wetu Yesu Kristo. Bwana Yesu Asifiwe!



**Mhariri  
anawataki  
wasomaji wote:**

**Heri ya Mwaka  
Mpya  
wenye Baraka.**

# Lutheran Uhuru Hotel and Conference Centre



Mandhari ya Kuvutia



Malazi Safi



Nyamachoma Maarufu



Vyakula vya Kikwetu na Kigeni

Kwa Mikutano, Semina, Harusi, Malazi, Mapumziko na Nyamachoma  
Pia Tunapeleka Wageni Mlima Kilimanjaro na Mbuga za Wanyama

*Ukhitaji Maelezo Zaidi, Wasiliana na Meneja*

**Lutheran Uhuru Hotel & Conference Centre**

P.O. Box 1320, Moshi, Tanzania: Simu: +255 272 754 084; +255 753 037 216

e-mail: [reservation@uhuruhotel.org](mailto:reservation@uhuruhotel.org); [manager@uhuruhotel.org](mailto:manager@uhuruhotel.org)

[www.uhuruhotel.org](http://www.uhuruhotel.org)

## Huduma za Uchapishaji

**Moshi Lutheran Printing Press ni kiwanda chako cha uchapishaji kinachoongoza kote kaskazini ya Tanzania kuhusu ubora, unafuu wa gharama, kasi na uaminifu. Tunachapisha:-**

**Vitabu, Kadi za kila aina, Majorida na Magazeti, Mabango, Vipeperushi, Bahasha, Hati za Fedha, Tikiti, Ratiba, Pakiti, Majalada, Daftari, n.k.**

Tunatoa huduma kamili za typesetting na usanifu.  
Tunakarabati vitabu vichakavu vikawa vipyta tena.  
Kwetu hakuna kazi iliyo ndogo mno au kubwa mno.  
Tunakushauri kuhusu kufanikisha malengo yako.

### *Fika Mara Moja*

**MOSHI LUTHERAN PRINTING PRESS**

**S.L.P 301, MOSHI, Simu: +255 272 750 546**

**E-mail: [lutheranpress@yahoo.com](mailto:lutheranpress@yahoo.com)**